

GREDI YA 4
MTIHANI WA MWISHO WA
MUHULA WA KWANZA 2023
KISWAHILI SEHEMU YA A

1. Ufahamu
2. Kusikiliza na Kuzungumza
3. Kusoma kwa sauti

Jina_____

Shule_____

Gredi_____

Jinsia

Mvulana_____ Msichana_____

KWA MATUMIZI YA MTAHINI

Tumia vigezo na viwango vya kuthaminia vilivyopewa kwenye mwongozo wa mwalimu.

	Kuzidisha Matarajio	Kufikisha Matarajio	Kukaribia Matarajio	Mbali Na Matarajio

ZOEZI LA KWANZA: UFAHAMU WA KUSOMA

A: KUSIKILIZA NA KUONGEA

1. Taja wanyama wawili wanaopatikana nyumbani (1)
2. Taja somo unalolipenda na kwa nini unalipenda somo hilo. (1)
3. Mwezi wa mwisho katika mwaka unaitwaje? (1)
4. Eleza tarehe mwezi na mwaka uliozaliwa. (1)
5. Je, unapenda chakula kipi zaidi? (1)

I. KUSOMA KWA SAUTI (dakika 1)

Kuna watu wengi ambao hupata riziki zao kupitia barabara. Mtu anaweza kuuza mazao ya shambani apate pesa. Anayenunua pia anaweza kuuza mazao hayo hayo kwa faida ambato itakuwa riziki yake. Mtu pia anaweza kuwekeza akiba yake katika mradi unaozalisha mapato zaidi. Mtu anaweza kutumia pesa alizohifadhi na kujenga nyumba ambazo watu watazikodi na kupata pesa baada ya wapangaji kulipa.

2.

Aida na Aisha ni mapacha. Wanafanana kama shilingi kwa ya pili. Wanatofautiana tu kwa kimo. Aida ni mrefu kama mlingoti na Aisha ni mfupi kama nyundo. Kila mmoja wao ana paka. Paka wa Aida no mweusi kama makaa. Yule was Aisha naye ni mweupe kama pamba. Paka wa Aisha anapenda kula chakula kingi. Amenona kama nguruwe. Yule wa Aida amekonda kama ng'onda.

a) Aida na Aisha ni _____ (1)

b) Paka wa nani anafanana kama makaa?

_____ (2)

c) Taja tashbihi tatu zilizotajwa kwenye hadithi.

(3)

d) kati ya Aida na Aisha yupi ni mfupi?

(2)

e) Ni mnyama yupi aliyetajwa katika hadithi?

(1)

ZOEZI LA PILI: MATUMIZI YA LUGHA

5. Tunga sentensi ukitumia maneno haya.

(5)

Runinga

Sebuleni

Meza

Neti

Makochi

Ambatanisha maamkuzi na maagano yafuatayo.

shikamoo	binuru
hujambo	nawe pia
alamsiki	aheri
masalkheri	marahaba

siku njema

sijambo

Andika wingi wa sentensi zifuatazo.

(5)

a) Soko limechafuka sana.

b) Jua limechomoza mapema






c) Kiti hiki kimevunjika

d) Mlango umefungwa

e) Samaki ameliwa

Tambua majina na mavazi haya.

(5)

Andika sentensi zifuatazo kwa wakati ujao.

(5)

a) Juma alisoma kitabu.

b) Mwalimu alisahihisha madaftari.

c) Mgeni alikaribishwa kwa furaha.

d) Tunaenda uwanjani kucheza.

e) Ninaenda shuleni.

